

Jinsi Wazazi Wanavyoweza Kuwasaidia Watoto Wao Kujifunza Lugha ya Pili

Wajifunzaji wa lugha zaidi ya moja wanajifunza lugha ya masomo na wakati huo huo wanasoma maudhui magumu ya kitaaluma, na hapo hapo wanajaribu kudumisha usawazo kati ya utamaduni wao wa kwanza na ule mpya ambao kwa sasa ndiyo wanaoutumia kujifunzia. Wazazi/walezi wanaweza kuwasaidia watoto wao kufanikiwa kwenye mazingira ya shule inayozungumza Kiingereza kwa kuwasaidia wanafunzi hao kujifunza kusoma na kuandika Kiingereza nyumbani. Jaribu kutumia mikakati hapo chini ili kumsaidia mtoto wako wa ELL awe na mafanikio ya kitaaluma si tu kwa lugha moja, bali mbalimbali.

- **Usiogope kutumia lugha yako asili.** Kidokezo hiki kinaweza kuwa cha muhimu zaidi kwa kuwa ni kiunganishi kati ya mazingira ya ujifunzaji ya mtoto wako – yaani, muunganiko kati ya lugha na utamaduni wake wa kwanza na lugha na utamaduni mpya. Unaweza kuyaelezea maneno na dhana mpya katika lugha anayoiuia mtoto wako na kuzidi kuendeleza stadi zake za kusoma na kuandika katika lugha ya kwanza, huku mkifanya mazoezi na kujifunza Kiingereza na ujifunzaji wa kitaaluma. Uwezekano wa ufanyaji mazoezi mara kwa mara na ufanyaji mazoezi yenye tija na uwekaji mkazo katika kujifunza lugha mpya na kuelewa utamaduni mpya ni mambo muhimu.
- **Linapokuja suala la kazi za shule, andaa ratiba.** Kuandaa ratiba nzuri ya kusoma nyumbani ni jambo linaloweza kuleta maendeleo makubwa katika ujifunzaji wa mtoto wako. Tengeneza mazingira yaliyo tulivu kwa kuondoa au kupunguza mambo yanayoweza kukengeusha fikra na hakikisha kwamba mtoto wako ana vifaa vyote anavyovihitaji ikiwemo penseli, vitabu, karatasi, n.k. Tenga muda wa kujibu maswali yoyote aliyonayo mtoto wako. Kama hujui majibu husika, unaweza kumsaidia mtoto wako kutafuta nyenzo za kumsaidia kujibu maswali aliyonayo, au unaweza kumsaidia mtoto wako kuyaandika maswali hayo ili akamuulize mwalimu wake. Hata kama wewe binafsi bado huwezi kuzungumza Kiingereza, unaweza kumkagua mtoto wako ili kuona kama kazi za shule zimefanywa.
- **Soma jambo lile lile kwa njia mpya.** Jaribu kusimulia hekaya au hadithi ya watoto ambayo wewe pamoja na mtoto wako mnaifahamu vizuri. Ingawa mwanzoni mtoto wako anaweza asiyaelewe maneno yote, kiujumla mtoto wako anapaswa kuelewa mtiririko wa hadithi na atajifunza msamiati na sarufi mpya kadri mtakavyoendelea. Kuuliza maswali yanayohusu mtiririko wa hadithi, wahusika, n.k., ni jambo linaloweza kuongeza uelewa wa mtoto wako. Mnaweza pia kujaribu kutazama filamu katika lugha mpya au hata kucheza michezo inayohusisha lugha, kama vile [Scrabble](#), ili kufanya mazoezi na kujifunza lugha nyumbani.
- **Tumia nyenzo za ubunifu kufanya mazoezi na kujifunza lugha.** Njia inayosisimua ya kufanya mazoezi na kujifunza lugha ni kufanya shughuli za ubunifu. Kwa mfano, tengenezeni pamoja kijitabu fulani na mjumuishe vitu vilivyopo kwenye nyumba yenu mpya, mji wenu mpya, na/au nchi yenu mpya na andikeni maelezo na vichwa vya habari kwa lugha yenu mpya. Je, mtoto wako anapenda kupaka rangi au kuandika? Mwambie achore picha na aandike au asimulie kisa kuhusu picha hiyo. Fursa zipo nyingi sana na zinategemeana tu na ubunifu wa mtoto wako.
- **Hamasisha ushiriki katika shughuli za baada ya masomo.** Shughuli za baada ya masomo, kama vile kuwa mwanachama wa gazeti la shule au kamati za kitabu cha mwaka cha shule, zinatoa fursa muhimu na za ziada za kujifunza lugha na kujua kusoma na kuandika. Shughuli kama hizi zinaweza kuwasaidia wanafunzi kuwianisha mitizamo, mikakati, wajibu na majukumu wanayojifunza darasani na yale ya nje ya darasa. Kuelewa na kutumia stadi za lugha na kujua kusoma na kuandika katika mazingira mbalimbali ni jambo muhimu katika kujifunza na ufaulu.
- **Wasiliana na shirikiana na walimu.** Ukiwa na taarifa wakati wote unaweza kwenda sambamba na maendeleo ya mtoto wako ya lugha, kitaaluma na kijamii shuleni. Kujua yanayojiri shuleni ni jambo litakalokupa uelewa mzuri zaidi wa jinsi unavyoweza kumsaidia mtoto wako nyumbani. Mapatano na ushirikiano kati ya shule na nyumbani huwasaidia watoto kufanya vizuri na kufanikiwa katika mazingira yao mapya ya ujifunzaji.

Chanzo: Edynn Sato, Ph.D.